TANGAZO LA SERIKALI Na. 279 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MIFUGO (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Mifugo (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2021 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za Mifugo za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka, 2014 ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya Tangazo La Serikali Na. 391 la Mwaka 2014

2. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (6) ambavyo vitasomeka;

4 (3) Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:

(a) Kuchunga, kulisha, au kunywesha mifugo katika maeneo ya ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) Kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) Kusafirisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine bila kibali cha kusafirisha mifugo;

(d) Kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(e) Kuuza au kununua mifugo katika eneo ambalo halikutengwa na Halmashauri kwa

ajili ya mnada, soko au gulio la mifugo;
(f) Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo.

(4) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu cha (3) (a) – (e) atakuwa ametenda kosa ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi 50,000/= kwa kila mfugo au kifungo cha miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(5) Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu kidogo cha (3) kipengele (f) atakuwa ametenda kosa ikidhibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi 200,000/= au adhabu ya kifungo cha miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(6) Wajibu wa mnunuzi wa mifugo:
(a) kununua mifugo katika eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya kuuzia mifugo;
(b) kulipia gharama zote zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na ada na ushuru kama itakavyopangwa na Halmashauri;
(c) kusafirisha mifugo pasipo kuiswaga barabarani;
(d) kutumia maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kupandisha mifugo kwenye vyombo vya usafiri;
(e) mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi Tsh. 50,000/= kwa kila mfugo au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

3. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (3), (4) na (5) ambavyo vitasomeka;

6 (3) Mfugaji atalazimika kuwa na kibali au vielelezo

vingine vinavyohusu mifugo hiyo wakati wote atakapokuwa anasafirisha mifugo yake;

(4) Kibali katika Sheria Ndogo hii kitakuwa na maana ya Mihtasari ya serikali za vijiji au na vibali vitakavyotolewa na Afisa Mifugo wa Halmashauri;

(5) Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu hiki atalazimika kulipa faini isiyozidi Shillingi Elfu Hamsini kwa kila mfugo au kifungo cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja.

4. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 7 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ambacho kitasomeka:

7 (3) Mifugo itakayokutwa ndani ya eneo la Halmashauri pasipo kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria Ndogo hii itakamatwa na kutozwa faini kiasi kisichozidi Elfu Hamsini kwa kila mfugo au kifungo cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja.

5. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kufuta kipengele (b) (c) na kuongezewa vipengele vidogo vipya vya 8(f) na (g) ambavyo vitasomeka:

8 (f) atashindwa kupiga chapa mifugo yake au mifugo yake itakamatwa na chapa ambayo haitambuliki na Halmashauri

(g) mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa ikithibitika atalipa faini isiyozidi Elfu hamsini, kwa kila mfugo au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja

6. Kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo Kuu kimefutwa na kuwekwa kipengele kipya ambacho kitasomeka:

9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi

laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili(12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yani fain na kifungo.

Marekebisho ya Jedwali

7. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo Kuu kwa kufuta Jedwali la kwanza na Jedwali la pili na kuweka Majedwali mapya na kuongeza Jedwali la Tatu kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

FAINI YA KUKOMBOLEA MIFUGO INAPOKAMATWA

| JINA LA MFUGO | KIASI KITAKACHOTOZWA |
|---|---|
| Ng'ombe | 10,000/= kwa kila mmoja |
| Punda | 5,000/= kwa kila mmoja |
| Mbuzi | 5,000/= kwa kila mmoja |
| Nguruwe | 5,000/= kwa kila mmoja |
| Kondoo | 5,000/= kwa kila mmoja |

JEDWALI LA PILI
TOZO YA MATUNZO YA MFUGO BAADA YA KUKAMATWA.

| JINA LA MFUGO | KIASI CHA TOZO |
|---|---|
| Ng'ombe | 5,000/= kwa kila siku mmoja |
| Punda | 4,000/= kwa kila siku mmoja |
| Mbuzi | 4,000/= kwa kila siku mmoja |
| Nguruwe | 4,000/= kwa kila siku mmoja |
| Kondoo | 4,000/= kwa kila siku mmoja |

JEDWALI LA TATU
TOZO YA KUOGESHA MFUGO

| JINA LA MFUGO | BEI YA KILA MFUGO (TSHS) |
|---|---|
| Ng'ombe | 500/= |
| Punda | 300/= |
| Mbuzi | 300/= |
| Kondoo | 300/= |
| Nguruwe | 300/= |
| Mbwa | 300/= |
| Paka | 300/= |

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2021 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2014 ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya Tangazo la Serikali Na.393 la Mwaka 2014

2. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 4 kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza vipengele vidogo vya (f), (g) na (h) ambavyo vitasomeka;

4(1) (f) Atatakiwa kuwa na mifugo iliyopigwa chapa inayotambulika na halmashauri kulingana na eneo mifugo ilipo;

(g) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu kidogo (1) (b) na (c) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi 50,000/= kwa kila mfugo au kwenda jela miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja;

(h) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu kidogo (1) (a), (d) na (e) cha kifungu hiki atakuwa

ametenda kosa ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi 200,000/= au kwenda jela miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

3. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 5 kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza kipengele (f) ambacho kitasomeka;

5(1) (f) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu hiki atakuwa ametenda kosa ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi 50,000/= kwa kila mfugo, isipokuwa akivunja kipengele (e) atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi 200,000/= au kwenda jela miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 6 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) cha Sheria Ndogo Kuu na kuweka kifungu kidogo kipya kama kifuatacho;

6 (2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini isiyozidi Shilingi 50,000/= kila mfugo, na gharama za kukamatwa na kukombolewa mifugo itakuwa kama inavyooneshwa katika Jedwali la II la Sheria Ndogo hii.

5. Kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo Kuu kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3), na (4)
ambavyo vitasomeka;

14 (3) Kila kaya inatakiwa kuwa na choo bora chenye sifa inayokubalika na kuhakikisha kinatumika;

(4) Kila kaya itakusanya taka katika chombo maalum ambazo zitakusanywa na Halmashauri kwa gharama kama inavyooneshwa katika Jedwali la IV la Sheria Ndogo hii;

6. Kifungu cha 20 cha Sheria Ndogo Kuu kinafanyiwa marekebisho kwa kuongezewa kifungu kidogo cha (2) ambacho kitasomeka;

20 (2) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yaliyo katika kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini kwa kila mfugo au kwenda jela miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

7. Marekebisho yanafanyika kwa kufuta kifungu cha 27 cha Sheria Ndogo Kuu na kuweka Kifungu kipya kitasomeka;

27 (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili yani faini na kifungo.

8. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo Kuu kwa kufuta Jedwali la II na III na kuengeza majedwali mapya kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA II

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 6(2))*

FAINI ITAKAYOTOLEWA KWA KILA MFUGO UTAKAOKAMATWA

| NA. | JINA LA MFUGO | KIASI CHA FEDHA TSH |
|---|---|---|
| 1 | NG'OMBE | 10,000/= |
| 2 | PUNDA | 5,000/= |
| 3 | MBUZI | 5,000/= |
| 4 | KONDOO | 5,000/= |
| 5 | NGURUWE | 5,000/= |

JEDWALI III

ADA YA MIFUGO KWA WAHAMIAJI KUTOKA NJE

Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5 (2)

| NA. | JINA LA MFUGO | KIASI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1 | NG'OMBE | 10,000/= |
| 2 | PUNDA | 5,000/= |
| 3 | MBUZI | 5,000/= |
| 4 | KONDOO | 5,000/= |
| 5 | NGURUWE | 5,000/= |

JEDWALI IV

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 14 (4))*

USHURU WA TAKA

| NA. | ENEO | KIASI TSH |
|---|---|---|
| 1 | KAYA | 1,500/= |
| 2 | DUKA REJA REJA | 2,000/= |
| 3 | DUKA LA JUMLA | 2,500/= |
| 4 | NYUMBA YA KULALA WAGENI | 3,000/= |
| 5 | TAASISI NYINGINE | 3,500/= |

Mabadiriko haya yanasomeka pamoja na Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi iliyobandikwa kwenye Marekebisho ya Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ya mwaka 2019 kufuatia azimio lililopitishwa na mkutano wa halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 28/2/2020. Na Nembo hii inabandikwa:-

MISSANA K KWANGURA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

SUMUNI ZENO MWANAKULYA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
3 Machi, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*